**MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA**

***Karatasi ya maswali: namba 5***

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada' unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

**MASOMO: 16- 19**

16. A. Sahihi au Kosa? Katika semi zifuatazo, amua ni zipi zinasema ukweli na zipi zimekosewa:
    - a) Mama wa Yesu alikuwa Mariamu.
    - b) Baba wa Yesu alikuwa Yusufu.
    - c) Yesu alikuwa mbinguni kabla ya kuzaliwa.
    - d) Mungu alijua tangu mwanzo kuwa angemtuma Yesu.
    - e) Yesu alikuwa na hulka ya kibinadamu (kama sisi) alipokuwa duniani.
    - f) Yesu anaitwa 'Mungu Mwana' katika Biblia.

Kazi ya ziada

B. Mpangilio wa sasa kulingana na **hadhi** ni huu:
Mungu – Yesu – malaika – mtu - wanyama.
Ni mpangilio upi uliokuwa kabla ya kifo cha Yesu? (Waebrania 2:9 inaweza kukusaidia)

17. A. Ni kwa namna gani Yesu alikuwa kama Mungu, Baba yake?
    B. Ni kwa namna gani Yesu alikuwa kama sisi?
    C. Kilichotokea ni nini wakati Yesu alipokuwa akijaribiwa nyikani?
    D. Tunaweza kujifunza nini kutokana na namna Yesu alivyoishi maisha yake?

Kazi za ziada

E. Yesu anasema nini katika Hotuba yake ya Mlimani juu ya:
- a) Talaka (Mathayo 5:32).
- b) Kuweka hazina (Mathayo 6:19-21).
- c) Kuhukumu wengine (Mathayo 7:1-5).
- d) Waalimu/Manabii wa uongo (Mathayo 7:15- 23).

F. Usome tena mfano wa Mpanzi (Mathayo 13: 1-8) na maelezo yake aliyotoa Yesu (Mathayo 13:18-23). Kama mbegu inasimama badala ya Neno la Mungu, yafuatayo yanawakilisha nini:
- a) Njia
- b) Miamba
- c) Udongo mzuri.

Tunajifunza nini kutokana na mfano huu?